


KUPANDA NDIZI KWA MBINU ZA KILIMO HAI



Kutumia kilimo hai katika kilimo cha ndizi kunachangia katika uzalishaji endelevu na udhibiti wa magonjwa na wadudu na huweza kuleta mavuno mengi

Kulingana na Shirikisho la kimataifa la harakati za kilimo hai (IFOAM, 2008), Kilimo-hai kinafanuliwa kuwa ni “mfumo wa uzalishaji ambao unaendeleza afya ya udongo, mifumo ya ikolojia na watu. Kilimo hiki hutegemea kwenye michakato ya ki-ikolojia, bioanuwai na mizunguko asilia ambayo inakubaliana na mazingira ya maeneo husika, badala ya kuingiza pembejeo ambao zina athari mbaya. Kilimo hai kinajumuisha utamaduni, ubunifu na sayansi ili kunufaisha mazingira tunayoshirikiana na kukuza mahusiano ya haki na maisha bora kwa wote wanaohusika”.


Utaratibu wa usimamizi wa bustani ya ndizi



Usimamizi sahihi huimarisha mimea na hupunguza kuenea kwa wadudu na magonjwa.

- > Weka mazalia 3 hadi 4 kwa shina
- > Ondo majani ya zamani kwani yanaficha magonjwa.
- > Acha majani 8 hadi 10 wakati mgomba unabeba, na 4 wakati wa kuvuna.
- > Tumia majani yaliyoondolewa kama matandazo.
- > Ondo machipukizi du me ili kumpunguza kuenea kwa ugonjwa.

Udhibiti wa magonjwa na wadudu



1. Tumia vifaa safi vya kupandia kwa ajili ya kuanzisha bustani mpya.



2. Ongeza mboji katika mashimo ya kupandia, weka mbolea ya kilimo hai juu na weka mabaki ya shamba kama matandazo.



3. Safisha vyombo na viatu au miguu kabla ya kuingia shamba lisilo na ugonjwa.



4. Bustani zilizoshambuliwa sana na magonjwa zifyekwe na kupandwa zao jingine.

Kilimo hai kinasisitiza kuzuia maambukizi na kuenea kwa wadudu na magonjwa.

- > Tumia aina zinazohimili magonjwa.
- > Tumia vifaa safi kwa ajili ya kupanda
- > Hakikisha usafi wa shamba.
- > Eneo kuzunguka shina lisiwe na kitu chochole.
- > Ongeza rutuba ya udongo.
- > Haribu mashamba yaliyojaa ugonjwa na usipande ndizi kwa mwaka 1 hadi 2.

Kuboresha rutuba ya udongo



Ongeza mboji kwenye shimo la kupandia



Mara kwa mara weka mboji na panda mazao yanayofunika ardhi



Weka matandazo au panda mazao ya kufunika ardhi

Hifadhi ya udongo na maji

- > Jenga uzio na panda mazao ya kufunika ardhi kuzuia maji kupotea na mmomonyoko wa udongo
- > Tumia miti ya kivuli na matandazo kuhifadhi unyevu wa udongo.

Mbolea za kilimo hai

- > Tumia mboji katika kupanda miche kwenye mashimo.
- > Ongeza mbolea kwa juu kabla tu ya kuchanua

Kilimo mseto cha ndizi na udhibiti wa magugu



Ndizi
Miti



vichaka vya miti jamii ya mikunde
Mazao ya kila mwaka



Kahawa/mti wa matunda
Mazao ya kila mwaka

Mfumo wa ghorofa

Ghorofa ya juu

- > Tumia miti ya kivuli kuinga dhidi ya upepo na kuzalisha mbao

Ghorofa ya kati

- > Panda miti ya matunda, kakao na kahawa kushamirisha uzalishaji wa ndizi.

Ghorofa ya chini

- > Panda mazao ya kila mwaka na mazao ya mikunde yanayofunika udongo
- > Kupalilia kwa muda stahiki huondoa ushindani wa magugu na magonjwa.

Utunzaji sahihi baada ya kuvuna na upatikanaji wa soko



Hakikisha mikungu
haianguki ardhani



Ndizi zilizovunwa zishughulikiwe
kwa uangalifu



Mikungu iliiovunwa
iwekwe kwenye kivuli na
isilundikwe pamoa

- > Hifadhi sahihi baada ya kuvuna huzuia ubora kupungua.
- > Mazao bora ya kilimo hai yana soko kubwa nje ya nchi.
- > Shirikianeni na wakulima wen-gine kupunguza gharama za uthibitisho.



Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development
and Cooperation SDC

Mchapishaji: TOAM kwa kushirikiana na FIBL. Kipeperushi hiki kinapatikana bure katika lugha za Kiswahili na Kiingereza kwenye tovuti: www.organic-africa.net/www.kilimohai.or.tz. Kimetasiriwa katika lugha ya Kiswahili na Dk. George M. Kiama (excelmercantile@yahoo.com). Tunawashukuru shirika la Uswisi linaloshughulikia maendeleo na ushirikiano (Swiss Agency for Development and Cooperation) Dar es Salaam kwa msaada waliooutoa kufanikisha tafsiri ya kipeperushi hiki. This flyer is freely available for download in both English and Swahili from www.organic-africa.net / www.kilimohai.or.tz.